## SURA YA KWANZA

# ASUBUHI YA DHAHABU

MAJIRA ya saa 12:00 asubuhi sauti za busara kutoka kinywani mwa ndege zilimfikia binti mrembo mwenye asili ya Singida. Binti ambaye siku alipozaliwa wazazi wake walimpatia jina la Balima kwasababu ya urembo wake. Siku hii ilimkuta Balima katika desturi za watoto ambao hawapendi kuamka asubuhi kwasababu ya uvivu.

Kwa vile alihisi kumepambazuka Balima alijisemea moyoni: ***"Ngoja nilalie mgongo dakika kadhaa wakati nikimsubiri mrembo wa baba atakapokuja kunikurupua kawaida yake ili nijiandae kwenda shule".***

Tofauti na siku zingine, siku hii Balima aliamka mapema sana na kupiga magoti kumuomba Mungu ayainue maisha yake na ya familia yake ambayo yaligubikwa na umasikini kiasi cha kutokuwa na uhakika wa milo mitatu kwa siku. Baada ya sala ya asubuhi Balima alijiegesha kitandani huku masikio yake yakiwa timamu kusikiliza vipindi mbalimbali vya redio vilivyokuwa vinaendelea redioni kutokea chumbani kwa wazazi wake.

*"Ilikuwa ni katika ukurasa wa kwanza wa gazeti la* ***SHEHENA*** *ulisomeka.....****Mwanamke wa kwanza kutoka Afrika aongoza mkutano wa wanawake duniani. Uingereza, Marekani na Australia zampigia saluti"***. Ilikuwa ni sauti iliyojaa udambwi udambwi wa kiutangazaji kutoka kwa mtangazaji wa Radio Free Afrika, kituo cha Dar es Salaam, Ahmed Ally akidonoa na kuperuzi kurasa mbalimbali za magazeti asubuhi.

Sauti ya Ahmed Ally kutoka katika redio ya mbao ya mzee Ikhuli ilifika barabara kabisa sikioni mwa Balima bila kuchujwa na kizuizi chochote. Ujumbe huo ulimfanya Balima kuanzisha mjadala kichwani mwake bila kuwa na wajumbe wala mwenyekiti kwa lengo la kumjua mwanamke aliyetajwa magazetini.

Kwa muda wa dakika kumi, Balima alikuwa anajiuliza maswali; *“Huyo mwanamke wa kiafrika ni nani? Ana cheo gani? Anatoka ndani au nje ya Tanzania? Amesomea wapi?”*

Balima alijua dhahiri kwamba sio rahisi kwake kupata majibu wala sauti ya kumpa tumaini la kujua chochote kuhusu maswali yake ingawa hali hiyo haiwezi kuwa kwasababu kwake kutojiuliza maswali. Balima alijua dhahiri kuwa wazazi wake hawakufanikiwa kwenda shule, lakini kwake hakikuwa kizuizi cha kufahamu jambo lolote kwa mawanda anayotaka. Siku hiyo Balima alipanga kumuuliza mwalimu wake wa darasa kuhusu huyu mwanamke aliyemsikia redioni.

*“Balima! Balima!..”* ilikuwa ni sauti ambayo aliijua sawasawa tangu alipozaliwa, ni sauti iliyomkuza katika malezi tangu akiwa tumboni, ilikuwa ni sauti ya mama yake mzazi. *“abee mama....",* niko macho mama najiandaa kwenda shule.”

*"Sawa mwanangu, jitahidi utachelewa..."* ilikuwa ni sauti ya kike yenye mkwaruzo uliosababishwa na kikohozi kikavu ambayo ilimsisitiza Balima kuamka na kujiandaa kwenda shule kwasababu ndiyo tumaini pekee lililokuwa limesalia katika safari ya ukombozi. Baada ya kumkumbusha binti yake, mama Balima alifunga mazungumzo yake kwa kihohozi kikavu kilichotuma ujumbe wa maumivu kwa kila sikio lililokuwa karibu yake.

Sauti ya kikohozi ilimuumiza sana Balima kiasi cha kutamani bora yeye angekuwa anakohoa badala ya mama yake ambaye ndiye muhimili wa mambo mengi katika maisha yao. Balima alijisemea moyoni huku macho yake yakilengalenga machozi *“Ningekuwa na pesa ningeenda dukani kumnunulia mama yangu walau vidonge vya rangi mbili ili ameze huenda atapona.......sasa hela nitatoa wapi? ......ngoja niende shule Mungu atamponya tu.”*

Baada ya kuvaa sketi yake chakavu yenye rangi ya bluu na shati jeupe ambalo lilionekana kubwa kwake, Balima alielekea jikoni kuangalia kama anaweza kupata chochote kitu ili kufungua kinywa. Alipiga hatua kama Ngamia mwenye njaa huku akichukua tahadhari zote ili asiparamie vyombo vilivyokuwa vimetapakaa kila kona ya jiko na kusababisha kelele ambayo ingesababisha

kuianza asubuhi kwa viboko badala kifungua kinywa kutoka kwa mama yake.

Akiwa jikoni, Balima aliangaza macho kwenye vyungu kadhaa jikoni bila kuona dalili za kupata chochote cha kutafuna huku kumbukumbu zake zikimkumbusha usiku walikula mihogo na karanga zilizokaangwa. Alipoona hakuna mafanikio ya kupata chakula chochote Balima, alienda mlangoni mwa chumba cha wazazi wake akaita na kusalimia kwa sauti unyonge *"Shikamoo baba! shikamoo mama!, ninaenda shuleni tutaonana baadaye nikirudi…..". "Haya mwanangu masomo mema ila kabla hujaondoka kuna mihogo ilibaki hapa usiku utaweka kwenye mfuko wa daftari utakula wakati wa mapumziko mwanangu",a*lisema baba yake baada ya kupiga chafya tatu mfululizo kabla ya kupokea salamu za mwanaye wa pekee, Balima.

Baada ya kupokea mihogo aliyoletewa na mama yake katoka chumbani, safari ya kwenda kutafuta elimu ilianza kwa tafakuri ya kitoto yenye mchanganyiko wa hasira na maumivu ya wivu baada ya kuwaona wenzake Nelson na Aviella kutoka katika familia za matajiri wakisubiri magari ya shule ilhali yeye anatembea umbali mrefu kila siku.

Hali hiyo ilimfanya Balima amfikirie baba yake kama kiumbe asiye na upendo na huruma. *"…kwanini mimi sifuatwi na gari nyumbani?, kwanini baba yangu hakunipeleka nikasome shule zenye magari na zinazofundisha kiingereza kama wanazosoma Nelly na Aviella?"* alinong'ona Balima kwa hasira kiasi cha kutoa sauti ambayo ilimfikia mama Minza ambaye anapishana naye njiani akiwa anaenda shambani kwake.

Sauti ya Balima ilimfanya mama Minza atafakari maumivu wanayopitia Balima na watoto wengine wanaotamani kusoma shule za binafsi zinazotoa huduma ya usafiri wa magari na zile zinazotumia lugha ya kiingereza lakini wazazi wao wanashindwa kumudu gharama kutokana na kuwa na kipato duni na umaskini uliokithiri.

Baada ya safari ndefu yenye maswali na vikao vya hapa na pale kichwani mwake, hatimaye Balima alifika shuleni. Huko nako alipokelewa na sauti za kuzomewa na wanafunzi wenzake Ibra na

Cally kwasababu ya miguu yake na sketi yake kutapakaa vumbi kutokana na kutembea umbali mrefu kutoka nyumbani kwao hadi shuleni.

Hali hiyo ilimwongezea Balima hasira...........